HOTUBA YA NAIBU KATIBU MKUU OFISI YA RAIS MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA, BW. HAB MKWIZU WAKATI AKIFUNGUA MKUTANO KUHUSU USHIRIKISHWAJI WA ASASI ZA KIRAIA KATIKA UFUATILIAJI WA HUDUMA ZITOLEWAZO NA SERIKALI, 05 NOVEMBA 2012

Ndugu Wakurugenzi wa Idara ya Utawala na Rasilimali Watu;

Wakuu wa Vitengo vya Mawasiliano Serikalini;

Wahariri kutoka Vyombo vya Habari Nchini;

Wawakilishi kutoka Asasi Zisizokuwa za Kiserikali: MISA Tanzania, TAMWA, HAKIELIMU, NOLA, UWAZI TWAWEZA, TANGO, SIKIKA NA TACOSODE;

Wanahabari;

Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana,

Habarini za Asubuhi,

Ndugu Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana,

Awali napenda nichukue fursa hii kukushukuruni nyote kwa kuhudhuria mkutano huu muhimu, hususan katika kipindi hiki ambacho Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma inatekeleza Awamu ya Pili ya Programu ya Mabadiliko katika Utumishi wa Umma.

Programu hii imejikita katika kuimarisha Uwajibikaji, Utendaji unaojali matokeo na inasisitiza ushirikishwaji wa Asasi za Kiraia ili wananchi ambao ni wadau wakubwa wa Serikali wapate huduma bora kutoka katika Taasisi mbalimbali za Umma hapa nchini.

Ninakushukuruni nyote kwa kutoa muda wenu ili kuhudhuria mkutano huu. Kukubali mwaliko na kufika kwenu kunaonesha ushirikiano mzuri uliopo kati ya Asasi zenu na Serikali na kutambua kwamba mkutano huu shirikishi ni sehemu ya mkakati mpana wa Serikali katika kuboresha utoaji wa huduma na kuwafikia wadau na wananchi kwa karibu zaidi. Kama mtakumbuka tulikutana mwezi Julai, 2012 kujifunza na kubadilishana uzoefu kuhusu ushirikiano baina ya Serikali na Asasi Zisizo za Kiraia.

Ndugu Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana,

Awamu ya Pili ya Programu ya Mabadiliko katika Utumishi wa Umma ni jitihada za Serikali za kuhakikisha kuwa Watanzania wanapata huduma zenye kiwango na bora kwa thamani ya fedha toka kwenye Serikali yao.

Mabadiliko yaliyotokea kati ya miaka ya 1980 na 1990, hususan Kisiasa, Kiuchumi na Kijamii katika nchi mbalimbali ikiwamo Tanzania yalisukuma Taifa letu kufanya mabadiliko katika utumishi wa Umma ili kukidhi mahitaji na wakati.

Kama inavyoeleweka Serikali ya Tanzania toka mwaka 1993 hadi 1998 ilitekeleza Programu ya Maboresho Serikalini (Civil Service Reform Programme) iliyolenga kupunguza ukubwa wa Serikali, kuweka mazingira mazuri ya ushirikishwaji wa sekta nyingine katika kazi ambazo hazikuwa lazima kufanywa na Serikali ili kuleta maendeleo nchini. Mabadiliko hayo yaliifanya Serikali kubaki na majukukumu machache.

Pamoja na hayo katika kipindi cha mwaka 2000 na 2007 Serikali ilitekeleza Awamu ya Kwanza ya Programu ya Mabadiliko katika Utumishi wa Umma (PSRP I) iliyoweka mifumo ya kiutendaji kwa lengo la kuimarisha huduma zinazotolewa na Serikali.

Kama nilivyotangulia kusema hapo awali hivi sasa Serikali inatekeleza Awamu ya Pili ya Programu ya Mabadiliko katika Utumishi wa Umma (PSRP II) ambayo imejikita katika kuhakikisha uwepo wa utendaji unaodhamiria uwajibikaji, unaojali na kuonyesha matokeo.

Ndugu Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana,

Lengo la Mkutano huu wa siku mbili ni kujenga uelewa wa pamoja juu ya utaratibu mpya unaoanza kutekelezwa na Serikali wa kushirikisha wananchi kupitia Asasi za Kiraia (AZAKI) ili kuimarisha utoaji huduma sahihi na bora kwa wakati muafaka, yaani huduma zenye viwango vilivyokubaliwa.

Mojawapo ya maeneo ya utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Programu ya Mabadiliko katika Utumishi wa Umma ni pamoja na ushirikishwaji wa Asasi za Kiraia katika kuboresha huduma kwa Umma.

Ushirikishwaji wa Asasi hizo ni mojawapo ya jitihada zinazofanywa na Serikali katika kuimarisha njia za mawasiliano na wananchi ikiwa ni pamoja na kuwahamasisha wadau wa Utumishi wa Umma au jamii kutoa taarifa pale huduma zinapokuwa na dosari au kutowafikia ipasavyo hivyo kudai huduma bora zaidi kutoka kwenye Taasisi za Serikali.

Hivyo Serikali kuzishirikisha Asasi za Kiraia katika kufuatilia na kufanya tathmini ya utoaji huduma italeta tija kwa Serikali kubaini kasoro au ubora wa huduma hizo. Aidha, mahusiano baina ya Serikali na Asasi hizo yatazidi kuimarika katika kuleta maisha bora kwa wananchi.

Ndugu Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana,

Ushirikishwaji wa Asasi za Kiraia katika kufuatilia huduma mbalimbali zitolewazo na Taasisi za Serikali ni mkakati wa mawasiliano ambao unapaswa kushirikisha Taasisi zote za Serikali ili kuwapa hamasa wananchi kutoa taarifa pale wanapoona wanapewa huduma zisizokuwa na viwango vilivyowekwa.

Najua wapo wenye shaka kuwa baadhi ya Asasi za Kiraia zinaweza zisifanye kazi kama ilivyokusudiwa, Kwa hali hiyo, ni muhimu kuwa na makubaliano kisheria na makubaliano kuhusu utaratibu na njia zitakazotumika kusambaza taarifa mbalimbali kwa wananchi.

Ni dhahiri kuwa Asasi za Kiraia zinayo nafasi kubwa katika kufuatilia huduma zitolewazo na Taasisi mbalimbali za Serikali na kubaini ubora wake, hususan kwa kuwashirikisha wananchi ambao ni wapokea huduma au walaji.

Iwapo fursa hii itatumika vizuri Asasi za Kiraia zitakua daraja imara kati ya watoa huduma ambao ni Taasisi za Serikali na wale wanaohudumiwa ambao ni wananchi. Hivyo huduma zitaendela kuwa bora na zenye viwango au kuwa bora zaidi. Njia hii ni shirikishi kwa sababu wananchi wataweza kuwasiliana moja kwa moja na Taasisi husika kuhusu huduma wanazopokea.

Ndugu Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana,

Yapo mengi mazuri yatakayopatikana pale Asasi za Kiraia zitakapofanya ufuatiliaji wa huduma mbalimbali zinazotolewa na Taasisi za Serikali kwa wananchi (Third party monitoring).

Moja ya faida hizo ni wananchi kutoa sauti zao moja kwa moja kuhusu huduma mbalimbali wanazopokea kutoka Serikalini. Jambo hili litasaidia kubaini ni Taasisi gani zinatoa huduma kwa kiwango kinachokubalika na wapi kuna matatizo ili yafanyiwe kazi.

Kwa ujumla Serikali inawapa fursa wapokea huduma kuongea wao wenyewe badala ya kusemewa kupitia mtu mwingine. Kupitia makubaliano na Asasi za Kiraia katika ufuatiliaji utoaji huduma kwa wananchi Serikali itakua inaimarisha uwajibikaji kwa wadau wake na uwazi katika kazi inazozitekeleza.

Ndugu Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana,

Mpango wa kuzishirikisha Asasi za Kiraia katika kufuatilia utoaji huduma wa Serikali tutakaojadili katika mkutano huu wa siku mbili utasaidia kueleweka zaidi kwa kazi mbalimbali zinazotekelezwa na Serikali kwa kuwashirikisha wananchi. Wananchi ambao ndio wadau wakuu wa Serikali watakua na nafasi pana ya kupima ubora wa huduma wanazopokea na kupendekeza ni wapi panapostahili kufanyiwa marekebisho ili huduma ziwe bora zaidi.

Ndugu Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana,

Nimeelezwa kuwa katika mkutano huu mada mbalimbali zitawasilishwa. Kwa maana hiyo mtapata nafasi ya kujifunza zaidi kuhusu namna ya kuzishirikisha Asasi za Kiraia katika ufuatiliaji huduma zitolewazo na Serikali. Hivyo mtafahamu Serikali inatakiwa kufanya nini, na nafasi ya Asasi za Kiraia katika kufanikisha lengo hili. Nia na madhumuni ya haya yote ni kuwa na uwazi, uwajibikaji, usikivu na Utawala Bora Serikalini. Ieleweke kuwa katika mukhtadha huu Asasi za Kiraia ni daraja baina ya wananchi na Serikali yao.

Naamini wote tunaohudhuria mkutano huu ni wadau muhimu katika suala hili, hivyo mawazo yenu ni muhimu kuhusu namna ya kushirikisha Asasi za Kiraia katika ufuatiliaji wa huduma zitolewazo na Serikali.

Ndugu Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana,

Naamini kuwa Asasi za Kiraia zikitumika vizuri wananchi ambao ndio wadau wakubwa wa Serikali wataweza kutoa sauti zao bila kupitia kwa mtu mwingine. Hii itasaidia kubaini Asasi za Serikali zinazotoa huduma ambazo zina mapungufu au kutokidhi viwango vilivyokubaliwa, pia baadhi ya watumishi ambao huwa kikwazo katika utoaji huduma. Hivyo ni jambo la msingi kabisa kuzishirikisha Asasi za Kiraia katika ufuatiliaji wa huduma mbalimbali zinazotolewa na Serikali.

Ndugu Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana,

Mwisho, napenda kuwatakia mkutano wenye mafanikio katika siku mbili mtakazokuwa hapa. Nina imani kuwa mtakuja na mipango na mikakati mizuri ya utekelezaji wa mpango wa ushirikishaji Asasi za Kiraia katika kuimarisha utendaji na Utawala Bora Serikalini.

Mabibi na Mabwana,

Baada ya kusema hayo napenda sasa kutamka kwamba mkutano huu umefunguliwa rasmi.

Asanteni kwa usikivu na nakutakieni Mkutano mwema, na wenye mafanikio kwenu na kwa Taifa kwa ujumla.